Pittsburgh Public Schools
Students first
Always, in all ways.

Ms. Dawn Golden
Assistant Superintendent,
Student Support Services

341 South Bellefield Avenue
Pittsburgh, PA 15213

studentservices@pghschools.org
412-529-3950

Septemba 22, 2025

Mpendwa Mzazi/Familia

Kama wilaya ya shule, tunaweka kipaumbele kwa walimu wetu na wafanyakazi wahusiane na wanafunzi ili kuhakikisha tunakidhi mahitaji yao ya kijamii na kihisia.

Mwaka huu, tunafanya kazi tena kuunganisha ujifunzaji wa kijamii na kihisia (SEL) katika ratiba na shughuli ambazo wanafunzi wanazifanya kila siku. Tunaendelea kutumia rasilimali kutoka Wayfinder, kwa kuzingatia nyenzo za msingi za Kujitambua, Kushirikiana, Kuonesha Huruma, Kukabiliana na hali mpya, Wakala na Kusudi.

Hatua nyingine muhimu tunayoichukua ni kutekeleza tena utafiti wa Mtazamo Mpana kwa Ustawi wa Wanafunzi na SEL kwa wanafunzi wote wa gredi ya 3-12 Mwanzoni mwa Oktoba (Oktoba 6-17). Uchunguzi huu majumui unatusaidia kuwaangalia wanafunzi wetu katika Wilaya yote.

Utafiti huo utatolewa mtandaoni kupitia shule ya mtoto wako. Utafiti huu utawauliza wanafunzi maswali yanayohusiana na stadi zao za kijamii na kihisia na ustawi, ikiwa ni pamoja na hisia nzuri na zenye changamoto, udhibiti wa mihemko, mikakati ya kijifunza, ufanisi binafsi, kujisimamia na uhusiano unaosaidia. Unaweza kuangalia nakala ya utafiti mtandaoni kwa kutembelea www.pghschools.org/SEL na kubofya kwenye kiungo cha “Utafiti wa SEL wa Mtazamo Mpana wa Mwanafunzi.”

Tutatumia taarifa tunazopokea kuwa na mazungumzo na kupanga usaidizi kwa ajili ya wanafunzi na kuongoza kazi tunayofanya katika ngazi ya shule na Wilaya. Utapata pia muhtasari wa ripoti. Tunapanga kutekeleza tena utafiti huu katika msimu ujao wa machipuo, ili kuendelea kufuatilia ustawi wa wanafunzi wetu.

Tafadhali mhimize mtoto wako ajibu kwa uaminifu kabisa. Utafiti huu ni wa hiari, na wanafunzi wanapaswa kujisikia huru kuruka swali lolote au wanaweza kuchagua kuacha kukamilisha utafiti. **Ikiwa hutaki mtoto wako akamilishe utafiti huu, tafadhali rudisha fumu iliyoambatishwa kwenye shule ya mtoto wako kufikia Jumatatu, Oktoba 6, 2025, au mjulishe mwalimu wa mtoto wako kwa simu au barua pepe.** Ikiwa una maswali kuhusu utafiti, tafadhali wasiliana na mkuu wa shule wa mtoto wako.

Asante,

Ms. Dawn Golden

Dkt. Rodney Necciai
Msimamizi Mkuu Msaidizi, Huduma za Usaidizi kwa Wanafunzi

www.pghschools.org
Parent Hotline:
412-529-HELP (4357)

The Pittsburgh Public Schools does not discriminate on the basis of race, color, age, creed, religion, sex, gender (including gender identity or expression), sexual orientation, ancestry, national origin, marital status, pregnancy, or disability in its programs. activities or employment and provides equal access to designated youth groups. Inquiries may be directed to the Assistant Superintendent of Student Services at 341 S. Bellefield Avenue, Pittsburgh, PA 15213 or (412) 529-HELP (4357).

Fomu ya Kujiondoa kwenye Utafiti wa Mtazamo Mpana

IKIWA **HUTAKI** MTOTO WAKO AKAMILISHE UTAFITI WA MTAZAMO MPANA, TAFADHALI RUDISHA FUMU HII KUFIKIA JUMATATU, OKTOBA 6, 2025. PIA UNAWEZA KUJULISHA MWALIMU WA MTOTO WAKO KWA SIMU AU BARUA PEPE.

Tafadhali weka utaratibu ili mtoto wangu asikamilishe utafiti wa SEL wa Mtazamo Mpana wa Mwanafunzi.

Jina la Mwanafunzi:
_____
_____

Gredi ya Mwanafunzi: _____

Jina la Mzazi/Mlezi: _____

Tarehe: _____